# MWONGOZO WA USAHISHAJI (CSSC)

# HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI- KIDATO CHA PILI MKONDO WA AMALI -AGOSTI 2025

**1.**

| I | II | III | IV | V | VI | VII | VIII | IX | X |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | B | D | D | C | B | C | B | C | D |

**Maksi01 @=maksi10**

**2.**

| I | II | III | IV | V |
|---|---|---|---|---|
| C | A | H | E | G |

**Maksi01 @=maksi05**

3. MTAHINIWA ANATAKIWA KUTAJA TUNU ZA TAIFA LA TANZANIA

i. AMANI: amani ni hali ya utulivu inayowezesha watu kuishi na kufanya shughuli zao kwa usalama.Tanzania imekuwa mfano wa nchi yenye amani katika Afrika kwa muda mrefu.Kuilinda amani ni jukumu la kila Mtanzania kwa kushirikiana na kuheshimu sheria.

ii. UMOJA: Umoja ni nguvu ya kitaifa inayojengwa juu ya mshikamano na ushirikiano bila ubaguzi.Pamoja na tofauti za kikabila na kidini, Watanzania wanaunganishwa na utambulisho wa taifa. Umoja unasaidia kujenga maendeleo endelevu na taifa lenye mshikamano wa kweli.

iii. HAKI NA USAWA:Haki ni kutoa au kupata kile mtu anachostahili kwa mujibu wa sheria na maadili.Usawa unahakikisha watu wote wanapata fursa sawa bila kubaguliwa. Utekelezaji wa haki na usawa huleta imani kwa serikali na taasisi za umma.

iv.UZALENDO:Uzalendo ni moyo wa kupenda nchi na kuwa tayari kuitumikia kwa uaminifu.Mzalendo huweka mbele maslahi ya taifa kuliko ya binafsi. Uzalendo hujengwa kupitia elimu ya uraia, historia ya taifa, na ushiriki wa maendeleo.

v. UADILIFU**:** Uadilifu ni kufanya mambo kwa uaminifu, haki, na kutofuata tamaa au rushwa.Mtu mwadilifu anaheshimu sheria na kutenda kwa misingi ya maadili mema. Uadilifu huleta imani kwa jamii na hujenga taasisi imara.

vi. UWAJIBIKAJI:Uwajibikaji ni kuwajibika kwa matendo, majukumu, na maamuzi yako binafsi au kitaaluma.Kiongozi au raia mwajibikaji hufanya kazi kwa bidii na uaminifu. Ni msingi wa ufanisi katika utawala bora na utoaji wa huduma kwa wananchi.
vii. UHURU: Uhuru ni haki ya mtu kufanya maamuzi au kuchagua bila shuruti, kwa kufuata sheria.Watanzania wana uhuru wa kutoa maoni, kushiriki siasa, na kujieleza. Hata hivyo, uhuru unaambatana na wajibu na mipaka ya kisheria.

viii. HESHIMA: Heshima ni kutambua thamani na utu wa mtu mwingine na kumtendea kwa adabu.Inahusisha kuheshimu wazazi, wakubwa, viongozi, na watu wote. Heshima hujenga jamii yenye utulivu, nidhamu, na mshikamano.

ix.UTU: Utu ni thamani ya msingi inayomtambulisha binadamu kama mwenye heshima nahaki.Kila mtu anapaswa kutambuliwa na kuheshimiwa kama kiumbe wa kipekee. Kudumisha utu ni msingi wa haki za binadamu na maisha yenye staha.

**Maksi02@=maksi10**

4. MTAHINIWA ANATAKIWA KUELEZA UMUHIMU WA SOMO LA H.T.M

i.Hukuza uzalendo na mapenzi kwa nchi:Kwa kuelewa historia ya taifa letu, tunajifunza thamani ya uhuru na amani tuliyonayo sasa.Somo hili humhamasisha mtu kuipenda nchi yake na kuwa tayari kuitumikia kwa moyo wa dhati. Uzalendo ni msingi wa mshikamano na maendeleo ya kitaifa.

ii. Hutufundisha maadili mema ya kuishi na watu wengine: Somo hili linasisitiza tunu na maadili kama uaminifu, heshima, uadilifu, na uwajibikaji.Maadili haya yanamwezesha mtu kuishi kwa amani na kuendana na jamii inayomzunguka.Mwanafunzi hujifunza kutofautisha kati ya mema na mabaya katika maisha ya kila siku.

iii. Kuelewa Asili ya Jamii za Kitanzania: Tanzania ina zaidi ya makabila 120, kila moja likiwa na historia, lugha, na mila yake.Kufahamu asili ya jamii hizi husaidia kutambua uzoefu wa kihistoria, namna walivyoishi, walivyopata maendeleo, na jinsi walivyoshirikiana kijamii na kiuchumi.

iv. Kuchambua maendeleo ya jamii za Tanganyika na Zanzibar kabla, wakati, na baada ya uhuru: somo hili linasaidia kujua na kuchunguza mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa yaliyotokea katika vipindi hivyo vitatu muhimu katika historia ya Tanzania.

v. Kuelewa tulipotoka tulipo na kutafakari kuhusu tunakotaka kwenda kama taifa:Kuelewa tulipotoka ni kutambua historia ya taifa letu, ikiwemo harakati za kupigania uhuru, misingi ya maadili, na jitihada za viongozi wa awali katika kujenga taifa lenye mshikamano. Kuelewa tulipo ni kuchambua hali ya sasa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

vi. kukuza maadili na utii wa sheria: Kwa kuzingatia maadili na historia ya taifa, mwanafunzi huwa tayari kuwa raia mwenye mchango chanya kwa jamii.Huchochea kufikiri kwa kina na kufanya maamuzi yenye kuzingatia maadili. Mwanafunzi hujengwa kuwa kiongozi bora, mwenye misimamo sahihi na anayejali maslahi ya wengi.

vii. kujenga utu na heshima: Somo hili linasisitiza tunu na maadili kama uaminifu, heshima, uadilifu, na uwajibikaji. Maadili haya yanamwezesha mtu kuishi kwa amani na kuendana na jamii inayomzunguka. Mwanafunzi hujifunza kutofautisha kati ya mema na mabaya katika maisha ya kila siku.

**Maksi02@=maksi10**

5. MTAHINIWA ANATAKIWA KUCHAMBUA VIPENGELE VYA KIUTAMADUNI VINAVYO TOFAUTISHA KABILA MOJA NA LINGINE

i.Lugha:Kila kabila huwa na lugha au lahaja yake ya kipekee ya mawasiliano. Lugha hizi huonyesha utambulisho wa kikabila na hutumika kufundisha mila. Zinaweza kutofautiana kwa matamshi, misamiati na sarufi.

ii. Mavazi ya Kitamaduni:Makabila huvaa mavazi ya kipekee yanayoakisi historia na utamaduni wao.Mavazi hayo hutumika hasa kwenye sherehe, matambiko na hafla za kijadi. Rangi, vitambaa na mapambo vina maana maalum kwa kila kabila.

iii. Chakula na Mila za Mapishi:Kabila lina vyakula vya asili na namna ya kipekee ya kupika.Mapishi hayo hutegemea mazingira na rasilimali zinazopatikana eneo hilo.Chakula huandaliwa kwa kuzingatia mila, hasa kwenye hafla maalum.

iv. Ngoma na Muziki wa Kitamaduni:Ngoma ni sehemu muhimu ya utambulisho wakabila, huambatana na ala za jadi.Midundo, nyimbo na mitindo ya kucheza hutofautiana kati ya makabila.Ngoma hutumika wakati wa furaha, ibada, matambiko au maombolezo.

v. Imani na Mila:Kila kabila lina imani za asili kuhusu uhai, kifo, mizimu na maumbile.Mila hizi huongoza maisha ya kila siku na kushikilia maadili ya jamii.Matambiko na desturi maalum hutekelezwa kwa kufuata imani hizo.

vi. Majukumu ya Kijinsia: Kuna mgawanyo wa kazi kati ya wanawake na wanaume kulingana na tamaduni.Majukumu haya huanzia kwenye familia hadi katika shughuli za kijamii.Katika baadhi ya makabila, mila huweka mipaka ya wazi ya kijinsia.

vii. Sanaa na Ufundi:Makabila hujulikana kwa aina fulani ya sanaa, kama vile uchongaji au ufinyanzi.Sanaa hutumika kufikisha ujumbe wa kihistoria au kiroho.Vitu kama vinyago, mapambo au vikapu huonyesha ustadi wa kabila fulani.

6. i.Kulinda jamii na mifugo: Morani huchukua jukumu la kuilinda jamii dhidi ya wanyama wakali na wavamizi. Wao hulinda maeneo ya malisho na kulala jangwani na mifugo. Ulinzi huu huonyesha ujasiri na umuhimu wao kwa jamii.

   ii. Kuwa walinzi wa utamaduni: Morani huvaa mavazi ya kitamaduni kama shuka nyekundu, mapambo na silaha za jadi. Wanazingatia mila zote kwa umakini na kuonyesha mfano kwa vijana wadogo. Wao huendeleza na kuhifadhi tamaduni za Kimasai kizazi hadi kizazi.

   iii. Kupigana na kulinda heshima ya jamii: Morani hupewa mafunzo ya kijeshi na kiufundi katika mapigano ya jadi. Wanatakiwa kuwa tayari kupigania heshima ya kabila lao. Kupambana na maadui wa jadi kulikuwa sehemu ya majukumu yao ya kihistoria.

   iv. Kujifunza uongozi na maisha ya utu uzima: Wakiwa morani, vijana hujifunza nidhamu, uongozi, na namna ya kuhudumia jamii.Hili ni daraja la kuandaliwa kuwa wazee wenye maamuzi siku zijazo. Malezi ya kiheshima na busara hujengwa katika kipindi hiki.

   v. Kuwa walimu wa vijana wengine: Morani huwahamasisha na kuwalea wavulana walioko chini yao kwa mila na desturi. Huwaonyesha jinsi ya kuvaa, kuzungumza na kuheshimu wakubwa. Hili husaidia kudumisha mshikamano wa kijamii na mwendelezo wa mila.

   vi. uchunga mifugo katika maeneo ya mbali: Wao huchunga ng’ombe katika maeneohatarishi au ya mbali kama sehemu ya mazoezi yaujasiri.Kuchunga huku huwafundisha ustahimilivu na umakini wa hali ya juu.Ni nafasi ya kujifunza kuhusu mazingira na maisha ya jangwani.

   vii. Kuwakilisha jamii katika mashindano na mikutano: Morani huwakilisha jamii yao kwenye mashindano ya kijadi, majadiliano au mabaraza.Hili huonyesha uwezo wao wa kuwasiliana na kuwakilisha maadili ya jamii yao.Ni nafasi ya kuonyesha umoja, heshima na utambulisho wao.

**Maksi02@=maksi10**

7. MTAHINIWA ANATAKIWA KUTAJA NJIA ZA KULINDA URITHI WA TANZANIA
   i.Kuelimisha Umma kuhusu Umuhimu wa Urithi: wanajamii wanapaswa kufundishwa thamani ya maeneo ya kihistoria na kitamaduni. Elimu hii inaweza kutolewa kupitia shule, vyombo vya habari, na makongamano. Ufahamu huongeza ushiriki wa jamii katika kulinda urithi wao.

ii. Matengenezo na Ukarabati wa Maeneo ya Urithi: Maeneo kama magofu, majumba ya kihistoria au mapango yanahitaji ukarabati wa mara kwa mara. Wataalamu wa kihistoria na usanifu wa majengo wanapaswa kushirikishwa. Hili huzuia maeneo hayo kuharibika au kupotea kabisa.

iii. Kuzuia Uvamizi na Ujenzi Holela:Maeneo ya urithi hayapaswi kuvamiwa kwa makazi au shughuli za kibinadamu.Mipango miji iendelee kulinda maeneo haya dhidi ya uharibifu wa maendeleo.Ujenzi usio rasmi huweza kuharibu thamani ya maeneo haya.

iv. Kuhamasisha Utalii Endelevu:Utalii unaolenga kuheshimu mazingira na historia huleta faida bila kuharibu maeneo.Mapato kutoka kwa watalii yanaweza kusaidia kutunza na kuendeleza maeneo hayo.Wananchi wa eneo husika wanapaswa kushirikishwa kwenye shughuli hizi.

v. Kuwashirikisha Jamii za Kiasili:Wenyeji wanaoishi karibu na maeneo ya urithi wanapaswa kuhusishwa moja kwa moja.Wao hujua historia ya maeneo hayo na wanaweza kusaidia kuyatunza kwa uangalifu.Kuwajengea uwezo na kuwapa motisha ni njia nzuri ya kuimarisha ushiriki wao.

vi. Kutumia Teknolojia ya Kisasa:Teknolojia kama sensa, kamera za ulinzi, na ramani za kidijitali husaidia ufuatiliaji.Maeneo yanaweza kupigwa picha za angani au kuchunguzwa kwa kutumia data.Hii husaidia katika kuhifadhi taarifa na kutoa tahadhari mapema dhidi ya uharibifu.

vii. Kufanya Tafiti na Utafiti wa Kihistoria: Wataalamu wa historia, akiolojia, na anthropolojia wanapaswa kuendelea kuchunguza na kubaini taarifa zaidi. Tafiti hizi huongeza maarifa na kusaidia kubaini maeneo yanayohitaji ulinzi zaidi. Pia huongeza kumbukumbu za kitaifa.

**Maksi02@=maksi10**

8. MTAHINIWA ANATAKIWA KUELEZA MAJUKUMU YA SERIKALI KATIKA UKUZAJI WA MAADILI NA UHIFADHI WA URITHI WA TAIFA

i.Kutunga na Kutekeleza Sheria za Maadili na Urithi:Serikali hutunga sheria zinazolinda maeneo ya kihistoria, utamaduni na mila za taifa.Mfano ni Sheria ya Mambo ya Kale ya 1964 inayolinda maeneo ya urithi wa kihistoria.Sheria hizi huweka adhabu kwa wanaovunja maadili au kuharibu urithi wa taifa.

ii. Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Maadili na Urithi:Kupitia shule, vyombo vya habari na semina, serikali hutoa elimu ya uzalendo, maadili na historia ya nchi.Lengo ni kujenga jamii

inayotambua na kuthamini maadili ya taifa na urithi wake.Hii hujenga kizazi kinachojivunia utambulisho wa kitaifa.

iii. Kufadhili na Kuwezesha Tafiti kuhusu Urithi wa Taifa:Serikali huunga mkono tafiti za kihistoria, utamaduni na kijamii zinazohusu urithi wa taifa.Hii husaidia kugundua na kuhifadhi maeneo mapya au maarifa ya kitamaduni.Tafiti hizo pia huimarisha mitaala ya elimu na kumbukumbu za kitaifa.

iv. Kuhifadhi Maeneo ya Urithi wa Kitaifa:Serikali hupitia taasisi kama TANAPA na Mamlaka ya Mambo ya Kale kulinda hifadhi na maeneo ya kihistoria.Inajenga miundombinu, inalinda mazingira na kuweka walinzi katika maeneo hayo.Hili husaidia kuhakikisha maeneo haya yanabaki salama kwa vizazi vijavyo.

v. Kuwekeza katika Utalii wa Kiutamaduni:Serikali huendeleza utalii unaolenga urithi wa taifa kama vile miji ya kale, mapango, na makumbusho.Mapato kutoka kwa watalii hutumika kuhifadhi maeneo hayo na kukuza uchumi.Pia, huchochea wananchi kutambua thamani ya maadili na urithi wao.

vi. Kushirikiana na Jamii katika Uhifadhi wa Maadili na Urithi:Serikali huunda sera zinazohusisha jamii za kiasili katika kulinda urithi wao.Jamii hushirikishwa kwa mafunzo, mikopo au miradi ya maendeleo ya urithi.Hii huongeza ushirikiano na kupunguza migogoro ya matumizi ya maeneo ya kihistoria.

vii. Kusimamia Vyombo vya Habari na Mitandao ya Kijamii:Serikali hudhibiti maudhui yanayopotosha au kushusha maadili ya taifa.Hutumika pia kuhamasisha uzalendo na kuelimisha kuhusu urithi wa kitaifa.Hili huzuia mmomonyoko wa maadili kupitia vyombo vya mawasiliano.

viii Kuhifadhi Lugha za Asili na Sanaa ya Jadi:Kupitia taasisi kama BASATA, serikali husaidia kukuza lugha na sanaa za asili.Hii hujumuisha mashindano ya sanaa, maonesho, na kutoa nafasi kwa wasanii wa kitamaduni.Ni njia mojawapo ya kuendeleza urithi usiogusika (intangible heritage).

ix. Kuweka Makumbusho na Kituo cha Kumbukumbu za Taifa:Serikali huanzisha makumbusho na majumba ya kumbukumbu kuhifadhi historia, picha na vifaa vya kale.Makumbusho haya huwafundisha raia na wageni kuhusu urithi wa taifa.Ni sehemu muhimu ya mafunzo na utalii wa ndani.

**Maksi02@=maksi10**

9. MTAHINIWA ANATAKIWA KUONYESHA UHUSIANO ULIOPO KATI YA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI NA MASOMO MENGINE

i.Uhusiano kati ya Historia ya Tanzania na Somo la Jiografia Historia inaelezea maendeleo ya jamii katika maeneo mbalimbali ya kijiografia, kama vile pwani na bara.Jiografia

husaidia kuelewa mazingira ambako matukio ya kihistoria yalitokea (kama vita, biashara, au ukoloni).Mambo ya historia kama harakati za ukombozi hueleweka vizuri kwa kuzingatia maeneo na rasilimali.

ii. Uhusiano kati ya Historia ya Tanzania na Masomo ya Lugha (Kiswahili & Kiingereza)Historia hutumika kama chanzo cha mada za kujadili au kuandika insha katika masomo ya lugha.Hujenga msamiati na uwezo wa kueleza matukio kwa mpangilio sahihi wa kihistoria.Masimulizi ya kihistoria huimarisha ufasaha wa lugha na uwezo wa kuelewa maandiko ya kihistoria.

iii.Uhusiano kati ya Historia ya Tanzania na somo laHisabati: Somo la Historia ya Tanzania na Maadili linahusisha matumizi ya takwimu na tafsiri zake kuhusu matukio ya zamani. Hisabati inaweza kutumiwa kuchambua takwimu za kihistoria na maadili. Vilevile, takwimu lazima ziwe na faida kwa binadamu na zifuate maadili ya jamii inayohusika, kwa mfano, kutunza siri za watu wakati wa kukusanya takwimu hizo.

iv. Uhusiano kati ya Historia ya Tanzania na somo la Chakula na Lishe: Somo la Historia ya Tanzania na Maadili lina uhusiano wa karibu na chakula na lishe kwa sababu huchangia katika kuelewa asili ya vyakula, mabadiliko ya mitindo ya kula katika jamii, na jinsi tabia za kula zinavyoathiri afya ya binadamu na mazingira.

v. Uhusiano kati ya Historia ya Tanzania na somo la Sanaa na Michezo: Sanaa na michezo ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Tanzania na inaathiriwa na historia na maadili ya jamii katika zama mbalimbali.

vi. Uhusiano kati ya Historia ya Tanzania na somo la Muziki: Muziki umekuwa sehemu ya historia tangu enzi ya mababu. Kupitia historia ya muziki, tunajifunza jinsi ambavyo muziki umekuwa chombo cha kuelimisha, kuburudisha, na kufahamisha kuhusu matukio mbalimbali ya kihistoria na maadili ya jamii.

vii. Uhusiano kati ya Historia ya Tanzania na somo la Kilimo: Somo la Historia ya Tanzania na Maadili lina uhusiano na kilimo kwa kuwa kilimo ni sehemu ya mila na desturi za jamii za asili za Kitanzania na za sasa.

**Maksi02@=maksi10**

10. MTAHINIWA ANATAKIWA KUFAFANUA NJIA ZA KUPAMBANA NA RUSHWA.

Mtahiniwa anapaswa kujibu swali hili kwa kuandika kwa kutumia mfumo wa insha na mgawanyo wa maksi ni kama ifuatavyo:

Utangulizi -**maksi 2.5**

Kiini cha swali -**maksi 02** kwa kila nukta moja

Hitimisho- **maksi 2.5**

Jumla -**maksi 15**

Utangulizi

Rushwa ni kitendo cha kutoa au kupokea kitu chochote cha thamani (kama pesa, zawadi au ahadi) ili kupata haki isiyostahili au kuharakisha huduma kwa njia isiyo halali. Ni tendo linalokiuka maadili na sheria, na linafanyika kwa siri kati ya wahusika wawili au zaidi.Watu hupokea au kutoa rushwa ili kuepuka adhabu, kushinda zabuni au kupata ajira bila sifa.Ni mojawapo ya changamoto kubwa katika utawala bora na maendeleo ya nchi. Yafuatato ni majukumu ya serikali katika kupambana na rushwa.

Kiini cha swali

Kutunga na Kutekeleza Sheria za Kupambana na Rushwa: Serikali hutunga sheria kali dhidi ya vitendo vya rushwa, kama vile Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCA). Sheria hizi hutoa mwongozo wa adhabu kwa wanaojihusisha na rushwa. Zinatoa msingi wa kisheria kwa taasisi kushughulikia kesi za rushwa.

Kuunda Taasisi za Kupambana na Rushwa:Serikali huanzisha taasisi maalum kama TAKUKURU kushughulikia masuala ya rushwa.Taasisi hizi huchunguza, kuzuia na kuelimisha umma kuhusu madhara ya rushwa.Zina mamlaka ya kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika.

Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Madhara ya Rushwa: Serikali huendesha kampeni za uhamasishaji kupitia vyombo vya habari, mashuleni, na kwa njia ya mikutano.Wananchi hufundishwa jinsi ya kutambua na kuripoti rushwa.Elimu hii huongeza uelewa na kuchochea ushirikiano wa jamii katika mapambano hayo.

Kuhakikisha Uwajibikaji wa Viongozi na Watumishi wa Umma: Serikali huweka mifumo ya ufuatiliaji na ukaguzi wa matumizi ya fedha na maamuzi ya viongozi.

Viongozi wasio waaminifu huchukuliwa hatua kama kufukuzwa kazi au kufikishwa mahakamani.Uwajibikaji huu hupunguza mianya ya rushwa katika utumishi wa umma.

Kulinda na Kuhamasisha Haki ya Kuripoti Rushwa:Serikali hutoa njia salama kwa raia kuripoti rushwa bila woga, kupitia simu, barua au mitandao.Watoa taarifa hulindwa kisheria dhidi ya madhara au kisasi.Hii huongeza uwazi na ushiriki wa wananchi katika mapambano.

Kushirikiana na Taasisi za Kimataifa Kupambana na Rushwa: Serikali hushirikiana na mashirika ya kimataifa kama UNDP, Transparency International, na Interpol. Ushirikiano huu huwezesha kubadilishana taarifa, mbinu, na kuwadhibiti watuhumiwa wa kimataifa. Hii huimarisha juhudi za kitaifa dhidi ya rushwa inayovuka mipaka.

Kuhakikisha Uwazi katika Manunuzi na Zabuni za Serikali: Serikali huweka mifumo ya zabuni wazi ili kuzuia upendeleo na utoaji wa tenda kwa rushwa. Taratibu kama GePG (Government e-Payment Gateway) na mifumo ya ugavi husaidia kuondoa mianya. Uwazi huu hupunguza nafasi ya rushwa katika miradi ya maendeleo.

Hitimisho

Kwa ujumla, serikali ina jukumu kubwa na la msingi katika kupambana na rushwa ili kulinda haki, maadili na maendeleo ya taifa. Kupitia utungaji wa sheria, elimu kwa umma, uwazi katika utendaji, na uundaji wa taasisi maalum kama Takukuru, serikali huonyesha dhamira ya dhati ya kutokomeza rushwa. Ushirikiano kati ya serikali, wananchi na wadau wa kimataifa ni muhimu kuhakikisha jamii yenye uadilifu, uwajibikaji na ustawi wa kweli kwa vizazi vya sasa na vijavyo.